SHUGHULI ZA KISWAHILI - CBC GRADE 3 TERM 3 EXAMS 2023

SEHEMU YA B:

SEHEMU YA TATU:

UFAHAMU

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali

Pombo ni rafiki yangu sana. Pombo yuko kwenye gredi ya tatu Mashariki. Yuko darasa moja mbele yangu. Amekuwa na kichwa kigumu kama paka. Ameanza kuwa na tabia mbaya, pesa zikipotea watu husema ni yeye.

Sasa amekuwa mdomo wazi, akipata kitu chochote kinacholiwa anatupa mdomoni mbiombio. Sharubati mdomoni, peremende mdomoni! Mimi na wanafunzi wenzangu tumemwogopa na kusema mtoto huyu tumbo lake halijai?

Leo hadhuhuri aliiba chakula cha mtoto mmoja wa gredi ya pili. Akaenda kula msalani bila hata kunawa mikono.

Baada ya muda mfupi Pombo aliona kweli tumbo lilianza kunguruma! Akaanza kuendesha na kulia kama mwana mbuzi.

1. Pombo yuko kwenye gredi ya ngapi? _____
2. Pombo ameanza kuwa na tabia gani? _____
3. Pombo alienda kula chakula msalani ili _____
4. Wakati aliumwa na tumbo Pombo alilia kama _____
5. Wingi wa neno "**chakula**" ni _____
6. Neno "**msalani**" iko na maana gani? _____
7. Adhuhuri ni wakati gani? _____

SEHEMU YA NNE: SARUFI

Andika kwa herufi kubwa

8. bata mzinga _____
9. chakula _____